**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

# MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

TAARIFA YA MKURUGENZI MKUU KWA WAANDISHI WA HABARI

- Ndugu Gerson Msigwa, Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali,
- Ndugu viongozi mbalimbali na maafisa kutoka Idara ya Habari Maelezo,
- Ndugu wanahabari kutoka vyombo mbalimbali,
- Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Baada ya shukrani hizo, natoa shukrani na pongezi kwa Msemaji Mkuu wa Serikali na timu yake kwa kuandaa mikutano hii inayotupatia fursa ya kuwaeleza wananchi jinsi Serikali yao inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inavyowatumikia na ilivyojipanga kuendelea kuwatumikia.

## 1. Utangulizi

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilianzishwa kwa Sheria Na. 3 ya Mwaka 2019 ili kudhibiti huduma za usafiri ardhini katika sekta za reli, barabara na waya. Sheria ya LATRA ilifuta Sheria Na. 9 ya mwaka 2001 iliyoanzisha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA).

LATRA ilianza kutekeleza rasmi majukumu yake tarehe 29 Aprili, 2019 baada ya Sheria yake kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 358 la tarehe 26 Aprili, 2019.

LATRA inaongozwa na Bodi ya wakurugenzi, Menejimenti inayoongozwa na Mkurugenzi Mkuu. Muundo wa Mamlaka una idara tano na vitengo vitano. Aidha, ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi, Mamlaka ina ofisi katika mikoa yote Tanzania Bara.

**Dhana ya udhibiti na uchumi**

Udhibiti ni njia mojawapo inayotumika na Serikali katika kusimamia uchumi wa nchi na kuendeleza ustawi wa jamii kwa kuhakikisha kwamba kwa huduma za msingi, mtumiaji analipa bei za haki. Hapa Tanzania dhana hii ilitokana na mabadiliko ya mfumo wa uchumi kutoka uchumi hodhi kwenda kwenye uchumi wa kati au uchumi mchanganyiko ambapo uwekezaji, uzalishaji na ugawaji wa bidhaa na huduma hutegemea upatikanaji wake na mahitaji ambapo bei za bidhaa na huduma hupangwa na soko lililo huru. Hivyo basi, ili soko hilo lisiachwe kabisa, Serikali ilitengeneza mfumo wa kiudhibiti bila kuathiri utendaji wake. Dhana hii kwa upana wake inahusisha uchumi mseto (mixed economy) ambapo Serikali hushirikiana na sekta binafsi katika kuendesha uchumi, hivyo basi Serikali inakuwa na wajibu wa kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji wa huduma mbalimbali.

Mwaka 1999 Serikali ya Tanzania, baada ya kubaini maeneo au huduma za kiuchumi zinazohitaji uangalizi ndani ya soko huru, iliandaa sera ya Ushindani na Udhibiti Huduma za Kiuchumi na Miundombinu. Sera hii ilipata kasi sana wakati wa ubinafsishaji wa mashirika ya umma. Hapo ndipo zilianzishwa Mamlaka mbalimbali za kiudhibiti ikiwemo (SUMATRA) ambayo baadae ikaja kuwa LATRA kwa ajili ya kudhibiti shughuli za kiuchumi katika sekta ya usfarishaji Ardhini.

## 2. Majukumu na Kazi za LATRA

Kifungu cha tano (5) cha Sheria ya LATRA kinaeleza kazi za Mamlaka, ambazo ni pamoja na:

a) Kutekeleza majukumu ya sheria za kisekta:

b) Kutoa, kuhuisha, au kufuta leseni:

c) Kwa mujibu wa sheria za kisekta:
   i. Kusimamia viwango vya ubora wa huduma na usalama katika sekta zinazosimamiwa
   ii. Kuweka vigezo na masharti ya utoaji wa huduma zinazodhibitiwa
   iii. Kudhibiti viwango vya tozo za huduma

d) Kuratibu shughuli za usalama wa usafiri wa ardhini;

e) Kusajili wahudumu na kuthibitisha madereva wa sekta zinazodhibitiwa;

f) Kuhakikisha kuwa treni na magari ya abiria yana ubora unaotakiwa;

g) Kufuatilia mwenendo wa utendaji kazi wa sekta zinazodhibitiwa kwa kuangalia kiwango cha uwekezaji, gharama za kutoa huduma, ufanisi na ueneaji wa huduma;
h) Kuwezesha utatuzi wa migogoro na malalamiko;

i) Kuelimisha umma kuhusu kazi na wajibu wa Mamlaka.

Kwa mujibu wa kifungu cha 6 cha Sheria ya LATRA katika utekelezaji wa majukumu yake, Mamlaka ina wajibu wa kuhakikisha kuwa inakuza ustawi wa jamii ya Watanzania kwa:

a) Kukuza ushindani na ufanisi katika sekta zinazodhibitiwa;
b) Kukuza usalama wa huduma za usafiri ardhini, wakiwemo watumia huduma;
c) Kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma hasa katika gharama za usafiri na ubora wa huduma;
d) Kuwalinda watoa huduma wenye ufanisi;
e) Kukuza upatikanaji wa huduma kwa watumiaji wote wakiwemo wenye kipato cha chini, watu wa vijijini na makundi maalum;
f) Kuelimisha umma kuhusu sekta zinazodhibitiwa, kazi na wajibu wa Mamlaka, haki na wajibu wa watumiaji, uwasilishaji wa malalamiko/migogoro na utatuzi wake; na
g) Kuzingatia uhifadhi wa mazingira.

Kwa ufupi LATRA, kwa mujibu wa Sheria namba 3 ya 2019 na Sheria za Kisekta, ni mdhibiti wa usafiri ardhini nchini kiusalama na kiuchumi, kwa maana ya;

- Usafiri wa barabara, Magari makubwa na madogo, pikipiki za miguu miwili (bodaboda) na mitatu (bajaji) yanayosafirisha abiria na mizigo kibishara
- Usafiri wa Reli, miundombinu ya reli na vyombo vinavyotumia reli.
- Usafiri wa Waya yaani ‘cable transport’
- LATRA imepewa jukumu la ujumla la kuratibu usalama wa usafiri ardhini na

### 3. Mpango Mkakati wa Miaka mitano 2020/21- 2024/25

Mpango Mkakati wa Mamlaka wa miaka mitano umejielekeza kuendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Ilani ya Chama Tawala, na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano uliojikita katika kujenga Tanzania ya viwanda kwa kuweka mazingira wezeshi ya ukuaji wa uchumi. Hivyo, Serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa katika miradi ya kuboresha miundombinu ikiwemo reli na barabara ili kurahisisha shughuli mbalimbali za kibiashara, kupunguza misongamano mijini na kuvutia uwekezaji.

**Maadili ya Msingi kwa watumishi wa LATRA**

a) Uwajibikaji

b) Uwazi

c) Uadilifu

d) Ufanisi

e) Uweledi

f) Utunzaji wa Mazingira

g) Ushirikiano

**Dira**

*“Kuwa mdhibiti anayeongoza barani Afrika, kwa huduma salama, shindani na rafiki kwa mazingira”*

**Dhamira**

*“Kudhibiti usafiri ardhini kwa kukuza ushindani, uwekezaji na matumizi ya teknolojia kwa huduma salama na zenye ufanisi kwa maendeleo endelevu nchini”*

**Mamlaka imejiwekea mpango mkakati wa miaka mitano, (2020/21- 2024/25), wenye malengo yafuatayo:**

(i) Kuimarisha programu za kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza katika sekta ya usafirishaji ikiwemo VVU/ UKIMWI
(ii) Kuimarisha mkakati wa kitaifa dhidi ya Rushwa na mpango wa utekelezaji
(iii) Kuimarisha uwezo wa Mamlaka kutekeleza majukumu ya kiudhibiti
(iv) Kukuza ushindani na ufanisi katika sekta ya usafirishaji
(v) Kuboresha uwezo wa kusimamia usalama wa usafiri ardhini
(vi) Kuboresha mazingira endelevu katika usafiri ardhini na
(vii) Kukuza huduma bora za usafiri ardhini

Ili kutekeleza malengo haya ipasavyo, Mamlaka imejipanga kuwafikia wananchi kupitia ofisi zake zilizopo mikoa yote Tanzania Bara na kutumia mifumo mbalimbali ya TEHAMA inayorahisisha utoaji wa huduma katika sekta zinazodhibitiwa.

## Usafiri kwa njia ya Barabara

Mamlaka inaendelea kuhamasisha matumizi ya vyombo vikubwa vya usafirishaji kwa lengo la kuongeza tija katika maeneo ya ubora wa huduma na gharama za usafiri. Hatua hii inahusisha utoaji wa elimu kwa wadau, kuhamasisha uwekezaji kwenye vyombo vikubwa vya usafiri na kuongeza ufuatiliaji kwenye maeneo yenye vyombo vidogo hususan vile vinavyotumika kinyume na kanuni. Kwenye jiji la Dar es salaam, tumeendelea kurefusha njia na kutoa leseni za magari makubwa yenye uwezo wa kubeba zaidi ya abiria 40 kwenye njia zote ndefu kwa lengo kuwapunguzia wananchi adha za usafiri na gharama za maisha.

Sambamba na kuhamasisha matumizi ya vyomo vikubwa, Mamlaka inaendelea kuhakikisha huduma za usafiri zinafika kwenye maeneo mbalimbali ya nchi. Mafanikio ya Mamlaka kwenye eneo hili yamechochewa na kuboreshwa kwa miundombinu ya barabara. Mamlaka imeandaa njia mpya za daladala kwenye maeneo mbalimbali hususan kwenye miji mikubwa. Katika Jiji la Dar es salaam njia mpya za daladala takribani 82 ziliandaliwa kwa ajili ya kupeleka mabasi kwenye masoko ya wamachinga kwa lengo la kuchochochea shughuli za kiuchumi kwenye masoko hayo.

Kwa ujumla kumekuwa na ongezeko la vyombo vya usafiri kila mwaka kwenye maeneo mbali mbali ya nchi. Mwaka 2021/22 idadi ya mabasi ya abiria yaliyopata leseni ni 47,547 na magari ya mizigo ni 143,011. Aidha, zimeandaliwa njia mpya ndefu za mabasi kama vile mabasi ya kutoka Songea kwenda Mwanza na kutoka Songea kwenda Kilimamnjaro.

Halikadhalika, kumekuwa na ongezeko la magari madogo ya kukodi ambayo yameongezeka kwa asilimia 821% kwa teksi za kawaida na asilimia 219% kwa teksi mtandao.

Katika kuimarisha udhibiti wa uvunjaji wa sheria na kanuni, Mamlaka imeunda kitengo maalumu kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa sheria na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili watumiaji wa huduma. Kero hizi ni pamoja na ukatishaji wa njia, upandishaji holela wa nauli, uendeshaji magari kwa mwendo kasi, unyanyasaji wa abiria hasa wanafunzi. Mamlaka imeendelea kuwahamashisha wananchi kutoa taarifa za vitendo vya uvunjaji wa kanuni kupitia namba yake mawasiliano isiyokuwa ya malipo ambayo ni 0800110019.

Kupitia kifungu cha 6(b) cha Sheria ya Na. 3 ya LATRA, Mamlaka ina wajibu wa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa ni salama. Mwaka huu wa fedha tumejipanga kutoa mafunzo kwa wamiliki wa magari pamoja na wasimamizi wao wa usafirishaji kuhusiana na masuala ya usalama. Eneo hili la usalama tunalisimamia kwa njia mbalimbali ikiwemo kufuatilia mienendo ya mabasi na madereva wake.

**Usafiri kwa njia ya Reli**

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini imepanga kuhakikisha usalama wa abiria na mizigo unazingatiwa katika usafiri wa reli. Hivyo Mamlaka itafanya kaguzi mbalimbali kwenye miundombinu ya reli za Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA) ili kubaini mapungufu yanayoweza kuhatarisha usalama wa treni. Kaguzi hizi zitaainisha vihatarishi vyote na kutengeneza mpango mkakati wa kurekebisha kwa lengo la kuziua matukio ya ajali. Maeneo yatayoangaliwa sana ni pamoja na madaraja, reli, mifereji ya maji, vifungashio vya reli, ushindiliaji wa kokoto kwenye tuta la reli na maungio. Hili ni jukumu kubwa kwa Mamlaka kuhakikisha ubora wa usafiri wa reli.

Kwa mujibu wa kifungu cha 60(m) cha Sheria ya Reli Namba 10 ya Mwaka 2017 pamoja na Kanuni zake, LATRA imepewa jukumu la kutoa ithibati ya miundombinu na vitendea kazi (rolling stock) kwa mradi mpya wa Reli ya Kisasa (SGR). Kwa kutekeleza takwa hilo la kisheria, Mamlaka imepanga kufanya ukaguzi maalum kwa ajili ya kuuthibitisha mradi wa SGR katika mwaka wa fedha 2022/2023. Hivyo mara baada ya TRC kupata vichwa na mabehewa, kazi hiyo itaanza mara moja.

Mamlaka, pia imepanga kutoa mafunzo kazini kwa Wafanyakazi Muhimu wa Usalama katika undeshaji wa reli (Safety Critical Workers) kwa TAZARA na TRC ili kuwaongezea ujuzi wa kutimiza majukumu yao kwa weledi. Mafunzo ya aina hii husaidia kuwafanya wafanyakazi hao muhimu kuzuia ajali zitokanazo na makosa ya kibinadam (Human Error). Tathmini inaonesha kwamba, makosa ya kibinadamu katika uendeshaji wa shughuli za reli huchangia asilimia zaidi ya 85% ya ajali za treni kwa TRC na TAZARA. Hivyo, kuendesha mafunzo hayo kutatatua kwa kiasi kikubwa ajali zitokanazo na makosa ya kibinadamu.

LATRA imepanga kuandaa kanuni za kutunza mazingira katika undeshaji wa reli. Ifahamike kwamba maeneo mengi ya ushoroba wa reli, hasa mijini yamesongwa na makazi ya watu ambao kwa kiasi kikubwa wamekaribia sana eneo la undeshaji wa reli. Kupitia kanuni hizo, maboresho yatafanyika kwa kuwashirikisha wadau muhimu wakiwemo wananchi na serikali zao za vitongoji/mitaa, namna bora ya kuhifadhi ushoroba wa reli bila kuharibu miundombinu. Kanuni hizi zitakuwa shirikishi kwa wadau wote wanaohusika.

Mamlaka itahakikisha usalama wa treni za mjini (Commuter Trains) unaimarishwa, hasa katika jiji la Dar es Salaam, ambapo TAZARA na TRC zinaendelea kutoa huduma ya usafiri huo. Mpango mkakati ni kuwa treni hizi za mjini zinaendeshwa kwa maboresho makubwa ikiwemo ubora wa siti, vitasa vya milango, vishikizi kwa abiria na taa za ndani ya mabehewa. Uwepo wa treni za mjini (Commuter) husaidia kupunguza msongamano kwenye mabasi ya daladala.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(g) cha Sheria ya LATRA Na. 3 ya mwaka 2019, Mamlaka itaendelea kuishauri serikali namna bora ya uendeshaji wa reli kwa njia iliyo salama na kuufanya usafiri wa reli kuwa wa kuaminika.

Aidha LATRA imepanga kuendesha semina mbalimbali kwa wananchi na wadau wanaotumia reli ili kuongeza uelewa wa usalama. Hili ni takwa la kisheria kama linavyoainishwa katika Kifungu cha 6(f) cha Sheria ya LATRA Na. 3 ya mwaka 2019.

## 4. 0 Kuboresha Utoaji wa Huduma kwa njia ya TEHAMA

Ili kuongeza ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu na mikakati yake, Mamlaka imeendelea kufanya uwekezaji kwenye matumizi ya mifumo ya TEHAMA. Mifumo hii pamoja na:

- Mifumo ya Ndani
- Mfumo wa Tiketi Mtandao
- Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari – VTS
- Mfumo wa Maombi ya Leseni kwa Mtandao – RRIMS na
- Mfumo wa Kutahini Madereva - DTS

### 4.1 Mifumo ya Ndani

LATRA inatumia mifumo mbalimbali ya ndani ya inayowezesha utoaji wa humuma kwa ufanisi na kwa wakati. Mifumo hii ni pamoja na Mfumo wa Upokeaji na Usambazaji wa Nyaraka, Mfumo wa Kielektroniki wa Mahudhurio, Mfumo wa Udhibiti Ukusanyaji Mapato (GePG), Mfumo wa Serikali Mtandao (eGA), Mfumo wa Uhasibu Serikalini (MUSE) na Mfumo wa Malipo ya Mishahara.

### 4.2 Mfumo wa Tiketi Mtandao

Kama tulivyowatangazia, mwezi huu wa Julai tumeanza rasmi matumizi ya tiketi mtandao kwa mabasi ya masafa marefu. Hadi sasa jumla ya mabasi 550 yameshaunganishwa kwenye mfumo wa tiketi mtandao ambayo kwa siku yanakatisha wasitani wa tiketi 5,000 – 7,000. Baada ya kikao cha tathmini tulichofanya kwa pamoja LATRA, TRA na TABOA tumeazimia kwa pamoja kuwa kufikia mwisho wa mwezi huu wa Julai mabasi yote yawe yameunganishwa kwenye mfumo na yanatoa tiketi za kieletroniki.

Matumizi ya tiketi za kieletroniki yamelenga kuwanufaisha wasafirishaji, abiria na Serikali. Kupitia mfumo huu wasafirishaji wanaweza kudhibiti mauzo ya tiketi kwa kuwa mfumo unawawezesha kuona mauzo yote yanayofanyika kupitia simu za mkononi. Nimatarajio yetu kuwa matumizi ya mfumo yatawawezesha wasafirishaji kuimarisha huduma zao kwa kuongeza uwekezaji kwenye sekta. Abiria watanufaika na matumizi ya mfumo kwa kuwezeshwa kukata tiketi kutokea mahali popote na kuepukana na adha za wapiga debe. Vilevile, Serikali itanufaika kwa taarifa zinazozalishwa na mfumo kwa kupata taarifa mbali mbali zitakazosaidia kufanya maamuzi muhimu yakiwemo ya kuberesha huduma, miundombinu na kukokotoa kodi ya mapato.

### 4.3 Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS)

Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) unaendelea kuboreshwa na sasa utamwezesha mwananchi kutambua mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mwendo wa gari kupitia ‘application’ maalumu ambayo itaanza kutumika kabla ya mwezi Septemba mwaka huu. Vilevile kupitia VTS tutakuwa na vituo vya taarifa kwenye stendi Kuu za Dodoma na Dar es salaam ambapo abiria watakuwa na uwezo wa kutambua mahali mabasi wanayoyasubiri yalipo. Kwa sasa VTS imeunganisha mabasi **7,502** na vichwa vya treni 36 kati ya hivyo 10 vya TRC na 16 vya TAZARA.

### 4.4 Mfumo wa Maombi ya Leseni kwa Mtandao – RRIMS

Tumefanya maboresho makubwa ya mfumo wetu wa kutolea leseni na kupanua wigo wake kwa kuufanya uwe ni mfumo unganishi kwa huduma mbalimbali zitolewazo na Mamlaka. Kupitia mfumo huu ambao kirefu chake kwa Kiingereza ni Railway and Road Information Management System (RRIMS), wateja wetu wanaweza kujisajili na kuomba leseni kutokea mahali popote. Baada ya kujisajili wanaweza kuingia kwenye mfumo na kupata huduma na taarifa mbalimbali zinazowahusu.

Kwa Mwaka huu wa fedha mfumo huu utaongezewa uwezo wa kuchukua taarifa zinazohusiana na huduma za usafiri wa reli ambazo ni pamoja na usajili wa vichwa vya treni, mabehewa na madereva. Kama mnavyofahamu reli yetu ya kisasa inakaribia kukamilika kwa kipande cha Dar es salaam – Morogoro, hivyo nasi wadhibiti tumejipanga kufanya kazi zetu kisasa.

### 4.5 Mfumo wa Kutahini Madereva (DTS)

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 5 (1) (e) cha Sheria ya LATRA, Mamlaka imepewa jukumu la kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu katika vyombo vinavyotoa huduma za usafiri kibiashara. Katika kutekeleza jukumu hilo, Disemba, 2020 LATRA ilianza rasmi kusajili madereva kwenye kanzidata na hadi kufikia Julai, 2022 madereva 10,324 wamesajiliwa.

Pamoja na kazi ya kusajili madereva kwenye kanzidata kuendelea, mfumo wa kutahini madereva umekamili na ulianza kutumika rasmi tarehe 1 Juni, 2022 ambapo hadi kufikia tarehe 22 Julai, 2022 madereva 90 wameshafanya mtihani wa kuthibitishwa. Mfumo huu unawezesha madereva kufanya mtihani na kusahihishwa kielektronic na kutuma matokea kwa muhusika kwa njia ya ujumbe mfupi wa maneno (sms).

## 5 Hitimisho:

Kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023 LATRA imejipanga kuhakikisha kuwa huduma bora na salama za usafiri ardhini zinawafikia wananchi, kuondoa kero na changamoto mbalimbali katika sekta. Hii ni katika kutekeleza maelekezo anayoyatoa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mara kwa mara.

Ili kutatua kero za wananchi kwa ufanisi, Mamlaka ina namba za simu katika kila mkoa Tanzania Bara ambazo mwananchi anaweza kupiga endapo atapata tatizo lolote au kuhitaji huduma ya Mamlaka. Vilevile, mwananchi anaweza kupiga simu bila malipo kupitia nambari 0800110019/20 masaa 24 siku zote.

Mamlaka imejipanga kusimamia huduma za usafiri ardhini ambapo huduma za usafiri wa barabara na reli zina mchango mkubwa katika kukuza uchumi na kuwezesha Tanzania kufanya biashara na Nchi za Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC).

Katika kutekeleza majukumu yake, Mamlaka inashirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo viongozi wa Serikali, waheshimiwa wabunge, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, na Kikosi cha Polisi Reli na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Aidha, Mamlaka imepanga kukusanya jumla ya Tzs. Bilioni 41.7 ambapo Mamlaka imejipanga kuchangia katika mfuko mkuu wa Serikali Tzs. Bilioni 6.3 kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwa ni pamoja na tozo za leseni na mtumizi ya mfumo wa Tiketi Mtandao.

Kabla ya kuhitimisha, ninapenda kutumia fursa hii kuwakumbusha watanzania wote tujiandae kuhesabiwa katika Sensa ya Watu na Makazi tarehe 23 Agosti, 2022. Matokeo ya sense hii yatasaidia kuboresha mipango ya usafiri na utoaji wa leseni kwa watoa huduma wa mabasi na daladala.

Baada ya kusema hayo, naomba niishie hapa kwa sasa, nawashukuru kwa usikivu wenu. Mimi na wenzangu tuko tayari iwapo kuna sehemu mtahitaji ufafanuzi.

Asanteni sana.

**CPA Habibu J. Suluo**

**Mkurugenzi Mkuu - LATRA**